**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents MoFP Budget

2015-06

# Hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Makadirio ya Mapato na matumizi 2015 - 2016

Tanzania, Jamhuri ya Muungano

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/233

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA,
# MHE. SAADA MKUYA SALUM (MB)
# AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16

**Dodoma** **JUNI, 2015**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/16.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote namshukuru Mwenyezimungu, mwingi wa rehma kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na afya njema ili kushiriki mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri uliyoiwezesha nchi yetu kufanya vema katika nyanja ya uchumi.

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya katika kipindi chote cha uongozi wako. Nakupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa busara za hali ya juu katika kutimiza majukumu yake.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia niwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima (Mb) na

Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu na pia kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya bajeti hii. Namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Servacius B. Likwelile, na Naibu Makatibu Wakuu Prof. Adolf F. Mkenda, Bibi Dorothy S. Mwanyika na Dkt. Hamis H. Mwinyimvua kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, ninapenda kuwashukuru Prof. Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na Bw. Rished Bade, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa. Ninawaomba wadumishe ushirikiano wanaonipa ili wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge wote, kwa kuendesha majadiliano ya bajeti ya mwaka 2015/16 kwa umakini tangu yalipoanza hadi sasa. Aidha, nawashukuru kwa namna ya pekee Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa. Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati katika kukamilisha uandaaji wa hotuba hii.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mhe. Dkt Grace Pujah (Mb) na Mhe. Dkt Innocent Seba

(Mb) kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kifo cha Mheshimiwa Kapt. John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Aidha, natoa pole kwa wananchi wote kwa ujumla kutokana na matukio ya ajali barabarani na maafa yaliyotokana na mafuriko makubwa yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**MAJUKUMU YA WIZARA**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Wizara ni pamoja na kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na ya nje pamoja na matumizi ya Serikali; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali; kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umaskini katika sekta mbalimbali; kusimamia Deni la Taifa; kusimamia upatikanaji wa rasilimali fedha zinazotumika katika miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi; kusimamia sera, sheria, kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa umma; kusimamia mali ya Serikali; kusimamia taasisi na mashirika ya umma; kusimamia masuala ya Tume ya Pamoja ya Fedha; kuandaa na kulipa mishahara ya watumishi wa Serikali; kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni ya wastaafu; na kudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2014/15 NA MALENGO YA MWAKA 2015/16**

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/15, majukumu ya Wizara yaliendelea kutekelezwa kupitia mafungu saba ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; na Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina. Aidha, utekelezaji wa Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi umejumuishwa katika hotuba hii kwa kuwa fungu hili huombewa fedha na Waziri wa Fedha.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/15 umezingatia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 - 2015/16; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); Malengo ya Maendeleo ya Milenia, 2015; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) pamoja na Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Vile vile, Mpango na Bajeti umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 pamoja na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now – BRN*).

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, pamoja na mambo mengine, Wizara ilipanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia sera za mapato na matumizi ya fedha za Serikali;
ii. Kusimamia udhibiti wa matumizi ya fedha za umma;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma;
iv. Kukamilisha Sera ya Taifa ya Mali ya Umma;
v. Kusimamia Ununuzi wa Umma;
vi. Kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma;
vii. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa MKUKUTA II;
viii. Kuendelea kuboresha huduma za pensheni kwa wastaafu na malipo ya mirathi;
ix. Kuandaa miongozo mbalimbali ya ukaguzi wa ndani;
x. Kufanikisha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu na ya kibiashara;
xi. Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya maafisa ununuzi na ugavi kwenye wizara, idara na taasisi zinazojitegemea nchini;
xii. Kukamilisha stadi ya kubainisha mwenendo wa uchumi na mapato ya muungano wa Tanzania;
xiii. Kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati;
xiv. Kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo ya Serikali; na
xv. Kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Wizara imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

**Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato**

**(a) Mapato ya Ndani**

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/15, sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 12,638.5 (ikijumuisha mapato ya mamlaka za serikali za mitaa). Hadi Aprili 2015, jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya mamlaka za serikali za mitaa) yalikuwa shilingi bilioni 8,924.9, sawa na asilimia 71 ya makadirio.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha ukusanyaji wa kodi, Wizara imeendelea kupitia sheria na taratibu mbalimbali kwa minajili ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na kupanua wigo wa kodi. Katika jitihada hizi, Wizara imefanikisha kupitisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2014 na sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2014.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:- kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali katika maeneo ya mapato yatokanayo na kodi na yasiyo ya kodi kwa kuanisha vyanzo vipya na kupanua wigo wa kodi; kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato; kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi; na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa kodi za majengo.

### (b) Usimamizi wa Misaada na Mikopo

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikisimamia na kuhakikisha ufanisi katika misaada tunayopokea kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika kuboresha ushirikiano kati ya

Serikali na Washirika wa Maendeleo, Wizara imeandaa rasimu ya Muongozo wa Ushirikiano yaani Development Cooperation Framework (DCF) ambao rasimu ya mwisho imekamilika na ipo katika hatua za kuidhinishwa na Serikali. Muongozo huu umezingatia maoni ya wadau wote ikiwa ni pamoja na Wadau wa Maendeleo, Wabunge, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Wanazuoni, na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Aidha, muongozo huu una masuala muhimu katika ushirikiano wa kimaendeleo ikiwemo namna ya kupokea fedha za maendeleo, uwajibikaji, masuala ya majadiliano pamoja na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Wizara itaandaa Mpango kazi wa kutekeleza DCF ili kuboresha ushirikiano kati yake na washirika wa maendeleo. Pia kufuatia kukamilika kwa DCF na kuidhinishwa, Wizara itasambaza DCF kwa wadau ili iweze kutoa muongozo wa ushirikiano. Ili kufanya muongozo huo kueleweka na kutumika kwa urahisi, Wizara itatafsiri DCF kwa Lugha ya Kiswahili pamoja na kuhakikisha eneo la Majadiliano linaboreshwa na kupatiwa muongozo kama DCF ilivyoelekeza.

**Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**19.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2014/15, Wizara imetekeleza yafuatayo: kuratibu uandaaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha 2015/16-2017/18 kwa wizara, idara zinazojitegemea, taasisi na wakala wa Serikali, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa na kusambaza kwa wadau; kuratibu vikao vya uchambuzi wa bajeti ya mwaka 2015/16 kutoka wizara, idara zinazojitegemea, taasisi na

wakala wa Serikali, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara imeandaa na kusambaza kwa wadau vitabu vya bajeti ya mwaka 2015/16 (Volume I, II, III & IV).

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na: kuandaa, kuchapisha na kusambaza kitabu cha tafsiri rahisi ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 yaani "Citizen's Budget"; kutoa mafunzo juu ya kuandaa mipango na bajeti kwa maafisa mipango, wahasibu na watakwimu 120 wanaoshiriki katika uandaaji wa mipango na bajeti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika wizara 3, idara zinazojitegemea 2, mikoa 16, mamlaka za Serikali za mitaa 49 na taasisi za Serikali 5 na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kuboresha Mfumo Mkakati wa Utayarishaji wa Mgawo wa Bajeti (Strategic Budget Allocation System) ili kurahisisha uandaaji wa bajeti ya Serikali kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2014/15 – 2016/17. Vile vile, Wizara iliratibu vikao mbalimbali na wadau wakiwamo Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kutathmini na kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo: kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali inayojumuisha matumizi mengineyo, mishahara na maendeleo; kupitia mfumo wa uwasilishaji wake na kuhakikisha kuwa

Sera na Mipango ya Kitaifa na ile ya Kisekta inazingatiwa ipasavyo; kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii; na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya uandaaji bajeti ili kukidhi mahitaji ya taarifa mbalimbali zinazohitajika.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaendelea kuzijengea uwezo wizara, idara za Serikali, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa katika uandaaji wa bajeti ya muda wa kati, usimamiaji wake na utoaji taarifa za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa wakati; kutayarisha taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti ya Serikali ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unazingatiwa; kufuatilia matumizi ya fedha za umma zikiwemo fedha za mishahara, matumizi mengineyo na fedha za Miradi; na kuimarisha uwezo wa Wizara katika kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

**Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa kutekeleza yafuatayo: kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 357 wa kada ya uhasibu, ugavi, na TEHAMA kutoka wizara, idara za Serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa; kusimamia ufungaji wa mfumo wa kielektroniki wa malipo ya kibenki - *TISS* na kuanza kutumika katika Hazina Ndogo zote nchini; kuandaa hesabu za majumuisho kwa kutumia viwango vya kimataifa - *IPSAS Accruals*; kuhakiki wastaafu wote wanaolipwa pensheni kupitia Wizara ya

Fedha; kuratibu utayarishaji hesabu na taarifa za Wizara na Idara zote za Serikali; na kusimamia uendeshaji mtandao wa malipo wa Serikali kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kuziwezesha wizara, idara za Serikali na mikoa kutumia mtandao kwa ufanisi.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zilizochukuliwa kuimarisha usimamizi wa fedha za umma ni kurekebisha sheria mbalimbali za fedha kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014. Aidha, Bunge lilipitisha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2014 na Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini ya Mwaka 2015. Katika mwaka 2015/16, Wizara itakamilisha muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali na marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina. Aidha, Wizara itakamilisha maandalizi ya kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Vituo vya Pamoja Mipakani.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma Wizara ya Fedha imeendelea kufanya ukaguzi wa ndani wa mara kwa mara kwa wizara na taasisi za Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara ilifanya uhakiki wa madai mbalimbali ya watumishi wa Serikali, watoa huduma na wakandarasi kabla ya kuyalipa. Wizara pia imetayarisha Miongozo ya Usimamizi wa Vihatarishi, Udanganyifu, Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani, Ufuatiliaji na Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi, Ukaguzi wa Ununuzi, na Ukaguzi wa Mikataba katika Sekta ya Umma. Miongozo hii itatumiwa na Wakaguzi wa Ndani na wadau wengine katika sekta ya umma ili kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji kazi.

**27. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara katika taasisi za Serikali; ukaguzi wa kiufundi katika miradi 21 ya maji, barabara na majengo katika mikoa ya Lindi na Mtwara na miradi 5 ya umwagiliaji iliyo chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa sasa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Katavi. Aidha, ukaguzi maalum wa Kituo cha Matibabu na Hospitali ya Kufundishia ya Chuo Kikuu Dodoma na malipo ya Pensheni katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali vilifanyika. Vile vile, Wizara ilifanya ukaguzi wa miradi 32 ya maendeleo katika mikoa ya Kigoma, Manyara, Dodoma, Mara, Mtwara na Dar es Salaam. Ushauri wa kuboresha mifumo katika maeneo husika ulitolewa.

**28. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imetoa mafunzo mbalimbali kwa wakaguzi wa ndani 354 na Maafisa 835 kutoka taasisi za Serikali kuhusu utumiaji wa mfumo wa uchambuzi wa kielektroniki (*IDEA Analytical software*), ukaguzi wa kiufundi, Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma, na ukaguzi unaozingatia maeneo yenye vihatarishi.

**29. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kutoa udhamini wa masomo kwa Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Wagavi na Wataalamu wa TEHAMA kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo wa Serikali; kuendelea kusimamia na kuratibu uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya kifedha ya Serikali; na kusimamia udhibiti wa

matumizi ya fedha za umma katika Wizara na Idara za Serikali kupitia mtandao wa malipo wa Serikali.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga pia kutekeleza yafuatayo: kutathmini Mfumo wa Orodha ya Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma; kufuatilia utekelezaji wa Miongozo ya Ukaguzi wa Bajeti na Mishahara; kukagua mfumo wa kuandaa Bajeti; kufanya ukaguzi maalum; kuchambua majibu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu na kuziwasilisha Bungeni.

**Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma**

**31.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2014/15 Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Programu hii imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na inatekelezwa katika maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto katika usimamizi wa fedha za umma kama ilivyobainishwa katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa programu hii umechangia kuboresha utendaji katika ofisi na wizara zifuatazo: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi;Wizara ya Mali Asili na Utalii; Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI; Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kuunganisha na kuhuisha mifumo ya kifedha ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha kwa wakati; kukamilisha mapitio ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali na kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu juu ya ukaguzi wa mifumo ya fedha, usimamizi na ukaguzi wa vihatarishi, ukaguzi wa bajeti na mishahara, ukaguzi wa miradi na matumizi ya mifumo ya kifedha.

**Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imekagua mafungu yote 49 ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu za Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara, Hesabu za Halmashauri zote 162 za Wilaya, Miji Manispaa na Majiji, Mashirika ya Umma 106, Balozi zote 32 zilizoko nje ya nchi, na Wakala 33 za Serikali. Ripoti zote za ukaguzi tayari zimewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukaguzi katika mashirika mengine yaliyobaki unaendelea na upo katika hatua mbalimbali.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi mkoani Dodoma umekamilika kwa zaidi ya asilimia 95 na muda wowote jengo hili litaanza kazi. Kwa kuanzia jengo hili litakuwa na ofisi nne ambazo ni Ofisi ya ukaguzi mkoa wa Dodoma, Ofisi ya Ukaguzi ya Bunge, Ofisi ya Ukaguzi TAMISEMI na Ofisi ya Ukaguzi kanda ya Kati.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yakayotekelezwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika jukumu la kukagua taasisi za Umoja wa Mataifa ambapo ofisi inaingia mwaka wa nne kuwa katika Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa (UN Board of Auditors); kuboresha mfumo wa ukaguzi kwa kutumia teknolojia ya kompyuta; kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuimarisha uwezo wao katika kutumia mfumo wa TeamMate na ili waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika ukaguzi wa kisasa; na kuendelea na uunganishaji wa ofisi za Ukaguzi zilizoko mikoani na makao makuu kwa kutumia *Wide Area Network*. Kwa kuanzia Ofisi 12 tayari zimeunganishwa.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2015/16 imepanga kutekeleza yafuatayo: kukagua mafungu yote ya Wizara, Mikoa, Halmashauri, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma; kuimarisha ukaguzi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; kuanza maandalizi ya kukagua sekta ya gesi, mafuta na madini kwa kuwajengea uwezo wakaguzi; na kuondoa wakaguzi katika majengo ya wakaguliwa katika wizara zote na katika mikoa yote kwa kuwaweka katika majengo yanayokamilika au ofisi mbadala za kupanga. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa wakaguzi wote hawatakuwepo katika ofisi za wakaguliwa ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Usimamizi wa Mali ya Serikali**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Mali ya Umma; na uthamini wa mali

ya Serikali katika mikoa nane na wakala moja. Aidha, Wizara iliendelea na zoezi la uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali kwa wizara, idara zinazojitegemea na wakala wa Serikali.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea na zoezi la kuondosha mali chakavu katika wizara na idara za Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 1.03 zilikusanywa kutokana na mauzo ya mali chakavu na utoaji wa leseni za udalali. Aidha, Wizara ilikamilisha uchambuzi na ufuatiliaji wa hasara zilizotokana na madawa na vifaa tiba kuisha muda wake wa matumizi kabla ya kutumika na mali nyingine za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 10.15 na ufutaji wa hasara hizo ulifanyika kwa Azimio la Bunge Na. 5/2014.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kukamilisha mkakati wa Sera ya Mali ya Umma; kufanya uthamini wa mali katika taasisi sita za Serikali; kuondosha mali chakavu, sinzia na zilizokwisha muda wake; na kuhakiki mali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali.

**Ununuzi wa Umma**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Wizara imetekeleza yafuatayo: kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 kwa taasisi za Umma 40 ambapo jumla ya watumishi 168 walihudhuria mafunzo hayo; kufungua ofisi mbili Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kati za Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; na kutoa mafunzo kwa asasi za

kiraia 25 kuhusu masuala ya ununuzi wa umma. Aidha, Wizara imeendelea kuhuisha taarifa za maafisa Ununuzi na Ugavi katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, na Pwani.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na maandalizi ya kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielekroniki (e-procurement system), Wizara imetoa mafunzo kuhusu mfumo wa upokeaji na usimamizi wa taarifa za ununuzi nchini katika vituo vya Mbeya, Arusha, Morogoro na Mwanza ambapo jumla ya washiriki 368 walipatiwa mafunzo ya mfumo huo. Jumla ya taasisi 379 zimepatiwa mafunzo na kuunganishwa kwenye mfumo huu, hii ikiwa ni sawa na asilimia 84 ya taasisi zote.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika usimamizi wa ununuzi kwenye Sekta ya Umma, Wizara imefanya ukaguzi wa taratibu za utoaji wa zabuni na utekelezaji wa mikataba itokanayo na ununuzi wa umma katika jumla ya Taasisi 76 zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea 17, Mashirika ya Umma 16 na Serikali za Mitaa 43. Ukaguzi huu umehusisha jumla ya Mikataba 4,532 yenye thamani ya shilingi bilioni 429.51. Maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu ni katika usimamizi wa mikataba na utunzaji wa nyaraka za zabuni.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma ya ununuzi Serikalini, Serikali imeanza utaratibu wa kununua magari kwa pamoja kwa lengo la kupunguza gharama ambapo hadi Aprili, 2015 jumla ya magari 179 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 10.197

yameagizwa. Hadi sasa mfumo huu wa ununuzi umeokoa kiasi cha Dola za Marekani 989,514.17 kwa magari 50 ambayo yameshawasili. Gari aina ya Toyota GX V8 ambalo lilikuwa linauzwa kwa bei ya Dola za Marekani 122,726.8 lilinunuliwa kwa dola za kimarekani 75,591.32. Gari aina ya Toyota Prado TX lilinunuliwa kwa Dola za Marekani 56,301.64 badala ya 77,754.84.

**44. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ilisajili na kuratibu mienendo na maadili ya wataalamu wa ununuzi na ugavi ambapo hadi Aprili, 2015 jumla ya wataalamu waliosajiliwa walikuwa 3,418. Aidha, Bodi ilikamilisha kuandaa mitaala mipya ya mafunzo ya taaluma itakayoanza kufundishwa mwaka 2015/16.

**45. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma iliendelea kusikiliza rufaa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa maamuzi yanatolewa ndani ya siku 45 kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011. Hadi Aprili 2015, jumla ya rufaa 21 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Kati ya hizo, rufaa tisa wazabuni walishinda, rufaa sita Serikali ilishinda, rufaa tatu zilifutwa kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria na rufaa tatu zilifutwa na walalamikaji wenyewe. Aidha, Mamlaka iliendesha semina kwa mikoa 10 ili kupata mawazo ya wadau wa ununuzi juu ya mfumo mzima wa uwasilishaji na ushughulikiaji wa rufaa. Mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Lindi, Mtwara, Tanga, Kilimanjaro Arusha, Katavi, Njombe na Manyara.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kukamilisha utekelezaji wa mpango kazi wa usimamizi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011; kuendelea kusimamia ununuzi katika sekta ya Umma; kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu sheria hiyo na Kanuni zake za Mwaka 2013; kuendelea na maandalizi ya kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki; kuendeleza kazi ya kufunga mfumo wa usimamizi na udhibiti wa mafuta katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya na Mwanza; na kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta katika vituo vya mikoa ya Iringa, Mbeya na Morogoro.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga pia kutekeleza yafuatayo: kufanya tathmini ya uthabiti wa mfumo wa ununuzi wa umma nchini; kujenga uwezo wa Maafisa Ununuzi na Ugavi Serikalini; kutekeleza mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma; kufanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013; na kuendelea na zoezi la kuhakiki taarifa za Maafisa Ununuzi na Ugavi waliopo Serikalini.

**Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2015, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imetekeleza yafuatayo: kuchambua bajeti za mapato na matumizi kwa taasisi na mashirika 133 yanayopokea ruzuku ya Serikali kwa lengo la kubaini taasisi na mashirika ambayo yanaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya Serikali; kuchambua Taarifa za Hesabu za Mashirika ya Umma 65 na kutoa mapendekezo

ya marekebisho stahiki kwa Bodi za Wakurugenzi na Wizara husika kwa lengo la kuboresha utendaji wa taasisi hizo; na kufanya uchambuzi wa Miongozo ya kiutendaji kwa taasisi na mashirika ya umma na kupitia kanuni za fedha 24, miundo ya utumishi 19, kanuni za utumishi nane, na mikataba ya hiari nane.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya kaguzi za Kimenejimenti katika Taasisi zifuatazo: *Rufiji Basin Development Authority (RUBADA);* Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP; *Tropical Pesticides and Research Institute (TPRI)*; na *National Ranching Corporation (NARCO).* Ushauri ulitolewa kwa ajili ya kuboresha usimamizi katika Taasisi hizo. Aidha, Wizara ilifanya uperembaji kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma 15 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti kulingana na Mikataba ya ununuzi. Mashirika hayo yaliyobinafsishwa ni pamoja na *Mwanza Textile, Shinyanga Meat, Ilemela Fisheries, Manawa Ginneries, Blanket Manufacturing, Mtwara Cashewnut Factory, Likombe Cashewnut, Newala I Cashewnut Factory, Newala II Cashewnut Factory, Mtama Cashewnut Factory, Mufindi Pyrethrum Factory, TTA Dabaga, Mufindi Tea Company, Ludodolelo Pyrethrum Factory* na *Mahenye Farm.*

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilitoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuongeza mtaji wa Benki ya Rasilimali - TIB; shilingi bilioni 50 - Kulipa Deni la PSPF (Pre-1999); Nyongeza ya Mtaji wa Benki ya Kilimo shilingi milioni 500; Malipo ya Pensheni kwa waliokuwa wafanyakazi wa Shirika la Simu - TTCL

shilingi bilioni 2 na Shirika la Posta - shilingi bilioni 1.74; TAZARA - shilingi bilioni 4.33; na shilingi bilioni 1.97 zililipwa kwa PPF ikiwa ni pensheni ya Wafanyakazi wa Vyuo vya Elimu ya Juu.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Ofisi ya Msajili wa Hazina itatekeleza yafuatayo: kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato yasiyo ya kodi kwa kuimarisha Mifumo ya upatikanaji taarifa kutoka katika Taasisi kupitia TEHAMA, kuwajengea uwezo watumishi katika maeneo ya uchambuzi wa kiufundi (*Technical Analysis*), Tathmini ya Kazi (*Job Evaluation*), Uchambuzi wa Taarifa za Fedha (*Financial analysis*), Uchambuzi wa Mikataba; kuendelea kuandaa Mikataba ya Utendaji na Bodi za Wakurugenzi na Watendaji wakuu kwa Mashirika na Taasisi zote, kufanya uhakiki wa Mali zilizoingizwa katika Daftari la Mali ya Mashirika na Taasisi za Umma, kufuatilia na kuhakiki mali zilizorithiwa kutoka Mashirika yaliyobinafsishwa ili kuziingiza katika Daftari la mali ya Mashirika na Taasisi za Umma; kufanya utafiti wa Taasisi zenye vyanzo binafsi vya mapato lengo likiwa ni kuangalia uwezekano wa kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

**Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Wizara iliendelea kushirikiana na wizara za ki-sekta katika kuendeleza progamu ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - PPP hapa nchini. Programu hii imejumuisha kutoa mafunzo ya dhana ya Ubia kwa Taasisi za Serikali ikwemo Mamlaka ya Bandari; Wakala wa Mabasi ya haraka –

DART; na Bohari Kuu. Aidha, Wizara imeendelea kutoa ushauri kwa Wizara na Taasisi mbalimbali hususani katika utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Matokeo Makubwa Sasa – BRN. Vile vile, Wizara imeshirikiana na wadau wengine kuandaa kanuni za sheria ya Ubia iliyofanyiwa marekebisho mwezi Desemba 2014.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 wizara imetenga fedha katika Mfuko wa kuwezesha Miradi ya Ubia – *PPP Facilitation Fund* – kwa ajili ya mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wanaochambua miradi ya Ubia na pia kuajiri Washauri – Elekezi katika miradi ya Ubia. Tayari wizara imepokea maombi kutoka Taasisi mbili za Serikali yaani TANROADS ili kugharamia Mshauri – Elekezi ( Transaction advisor) wa mradi wa Barabara ya Tozo ya Dar es Salaam hadi Chalinze; na kutoka Bohari Kuu kwa ajili ya kugharamia Mshauri – Elekezi wa mradi wa madawa muhimu. Wizara imeendelea kuchambua maombi hayo ili kujiridhisha kiasi halisi cha fedha zinazohitajika kabla ya kuziwasilisha kwa Taasisi hizo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Wizara itaendelea na jukumu lake la kisheria kuchambua miradi ya ubia itakayowasilishwa na kituo cha Ubia Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kwamba miradi hii ina tija kwa Taifa; inakuwa endelevu; na pia haiongezi deni la Taifa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri kwa wizara na Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba miradi bora inaibuliwa na kuendelezwa.

**Uratibu wa Utekelezaji wa MKUKUTA**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA, Wizara imetekeleza yafuatayo: kuandaa Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA II ya mwaka 2013/14; kuandaa Taarifa ya Maendeleo ya Malengo ya Milenia ya mwaka 2014; na kuendelea na utayarishaji wa Mfumo wa Taifa wa Kinga ya Jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imeanzisha mapitio ya MKUKUTA II na maandalizi ya mkakati mwingine. Vile vile, Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kimataifa ya kuandaa malengo ya maendeleo endelevu (Sustainable Development Goals 2030).

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuwafikia wajasiriamali wadogo wadogo hasa vijijini, Mfuko wa SELF umeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Aprili 2015, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.74 ilikopeshwa kwa wajasiriamali wadogo wadogo 2,834, kati yao 1,559 sawa na asilimia 55 ni wanawake na wanaume ni 1,275 sawa na asilimia 45. Katika idadi hii ya wajasiriamali vijana ni 856 sawa na asilimia 30. Aidha, kwa wastani urejeshaji wa mikopo ya Mfuko wa SELF umeendelea kuwa wa ufanisi katika kiwango cha asilimia 93 hivyo kuwezesha fedha za mfuko kuzunguka na kuwafikia wajasiriamali wengi.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2015/16 Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kukusanya na kuchambua taarifa mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali ili kuandaa taarifa ya mwisho ya utekelezaji wa MKUKUTA; Kukamilisha Mfumo wa Kinga

ya Jamii ikiwa ni pamoja na kuandaa muundo wa viashiria vya upimaji; na kuratibu mkutano wa kitaifa wa kujadili sera za kupambana na umaskini nchini. Aidha, Wizara kupitia Mfuko wa SELF imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 18; na kuendesha mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa mikopo kwa wajasiriamali 800 na wasimamizi 40 wa huduma za ushirika.

**Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu - FIU imepokea na kuchambua jumla ya taarifa 98 zinazohusu miamala shuku ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Aidha, taarifa 21 za kiintelijensia zimewasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na uchunguzi. Aidha, ukaguzi umefanyika kwa watoa taarifa ambao ni benki 15, kampuni za bima nne na *Casino* moja. Wizara pia imeandaa mwongozo wa ukaguzi utakaotumika wakati wa kukagua watoa taarifa.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha, kupitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) ilikagua benki za Stanbic na Mkombozi kuhusu suala la ESCROW ACCOUNT. Taarifa ya kiintelijensia iliyotokana na ukaguzi huo iliwasilishwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Hii ni kulingana na matakwa ya sheria ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano katika udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kubadilishana

taarifa za kiintelijensia na vitengo vya kudhibiti fedha haramu duniani, Wizara ilijiunga na Umoja wa Vitengo vya Kudhibiti Fedha Haramu Duniani. Aidha, Wizara imesaini Hati za Makubaliano na vitengo vya kudhibiti fedha haramu vya Angola, Kenya, Zambia na Uganda na hivyo kufikisha idadi ya hati nane za makubaliano na vitengo mbalimbali. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali na vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria vya Tanzania Bara na Zanzibar ambapo washiriki 99 walipata mafunzo.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kuwasilisha taarifa za kiintelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; kuratibu zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi nchini; na kutekeleza mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

**Tume ya Pamoja ya Fedha**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imeendelea kufanya Stadi ya Uhusiano wa Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano ambayo lengo lake ni kubaini mwenendo wa Mapato ya Muungano kutokana na ukuaji wa uchumi; na kushauri njia bora ya kuimarisha Mapato hayo. Aidha, Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mfumo bora wa uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) umeandaliwa na upo katika

hatua ya maamuzi. Maamuzi ya Serikali kuhusu waraka huu ndio yatawezesha kufunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja kati ya SMT na SMZ. Vile vile, Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha mapendekezo ya kufanya Stadi ya Uwekezaji Katika Mambo ya Muungano.

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kukamilisha taarifa za stadi ya uhusiano wa mwenendo wa uchumi na mapato ya Muungano na kuiwasilisha katika pande mbili za Muungano. Aidha, Tume inakusudia kuendelea kufanya stadi ya uwekezaji katika mambo ya Muungano. Stadi hii inalenga kubaini ushiriki wa pande mbili za Muungano katika uwekezaji kwa mambo ya Muungano.

**Mpango wa Millenium Challenge Account- Tanzania**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Serikali ya Tanzania kukidhi vigezo na kuchaguliwa na MCC kunufaika na msaada wa awamu ya pili, maandalizi ya mpango huu wa pili (compact II development) yalianza Aprili 2013 na yatakamilika Septemba 2015. Aidha, mwezi Novemba 2014, Serikali ya Marekani ilitiliana saini na Serikali ya Tanzania mkataba wa kutoa Dola za Marekani milioni 9.78 za kugharamia baadhi ya kazi za maandalizi ya miradi iliyopendekezwa, hususan upembuzi yakinifu na usadifu katika miradi ya umeme kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi,2015 Dola za Marekani milioni 2.34 zilikuwa zimetolewa na kutumika kwa ajili ya upembuzi yakinifu

na usadifu wa miradi hii ya umeme. Kazi hii inaendelea na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2015, ambapo makadirio ya gharama za mpango huu zitabainishwa kwa maandalizi ya mkataba wa ufadhili wa miradi hiyo.

**Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuboresha huduma za pensheni zinazotolewa moja kwa moja na Wizara yafuatayo yametekelezwa: kuhakiki idadi halisi ya wastaafu ambapo hadi Aprili, 2015 jumla ya wastaafu 2,273 walihakikiwa na kumbukumbu zao kuingizwa kwenye daftari. Idadi hii inafanya jumla ya wastaafu walioingizwa kwenye daftari kufikia 62,126. Aidha, kumbukumbu za wastaafu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA ambapo kumbukumbu za wastaafu 17,286 ziliwekwa kwenye mfumo huo.

**Mifuko ya Hifadhi za Jamii**

**Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2015, Mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 518.13 ambapo kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 334.24 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 183.89. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 530.38 zilitumika kulipa mafao ikiwa ni pamoja na mafao ya kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi kwa wanachama 6,653. Vile vile, Mfuko ulizindua huduma za Fao la Uzazi, Mkopo wa

Elimu na Mkopo wa Kujipanga Kimaisha ili kuboresha maisha ya wanachama.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 891.76. Kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 645.81, na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 245.95. Aidha, Mfuko unatarajia kulipa kiasi cha shilingi bilioni 854.38 kwa ajili ya mafao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi, ambapo jumla ya wanachama wapatao 5,445 wanatarajia kustaafu kwa mujibu wa sheria. Vile vile, Mfuko unatarajia kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 110.59 kwenye maeneo mbalimbali ya vitega uchumi.

**Mfuko wa Pensheni wa GEPF**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2015 Mfuko umesajili jumla ya wanachama 13,093 kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi. Michango ya wanachama ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 36.45 sawa na asilimia 86.56 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 42.11. Mapato yatokanayo na vitega uchumi yalifikia shilingi bilioni 26.34 ambayo ni sawa na asilimia 74.91 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 35.10. Thamani ya Mfuko ilikua na kufikia shilingi bilioni 328.8.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Mfuko utaendelea na jitihada za kuboresha huduma kwa wanachama kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano, kupanua wigo wa wanachama na kukuza mapato yatokanayo na uwekezaji. Mfuko unatarajia kusajili

jumla ya wanachama 24,020 na kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 62.21. Aidha, mapato ya vitega uchumi yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 36 na thamani ya Mfuko inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 537.08.

**Mfuko wa Pensheni wa PPF**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014, idadi ya wanachama wapya walioandikishwa ilifikia 67,302 ikilinganishwa na 63,582 mwaka 2013. Michango ya wanachama iliyokusanywa na mfuko ilifikia shilingi bilioni 335.7 sawa na ongezeko la asilimia 20.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 278.5 zilizokusanywa mwaka 2013. Ongezeko hili limechochewa na kuongezeka kwa mishahara ya wanachama, waajiri kuzingatia sheria kwa kuleta michango kwa wakati pamoja na uandikishaji wa wanachama wapya. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 318 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 361.7 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.7. Thamani ya Mfuko imeongezeka na kufikia shilingi trilioni 1.96 ikiwa ni ongezeko la asilimia 32 ikilinganishwa na thamani ya Mfuko ya shilingi trilioni 1.49 iliyokuwa mwaka 2013. Vile vile, Mfuko ulilipa jumla ya shilingi bilioni 156.4 kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na shilingi bilioni 131.9 zilizolipwa mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 18.5.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 657.3, kati ya hizo michango ya wanachama ni shilingi bilioni 400 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 257.3. Aidha, thamani ya Mfuko inatarajiwa

kufikia shilingi trilioni 2.35. Vile vile, Mfuko unatarajia kuandikisha wanachama wapya 87,000.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na yaliyotokana na wastaafu wa kabla ya mwaka 1999, Serikali iko katika mchakato wa kutoa hatifungani ya muda mrefu yenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 kwa mifuko hiyo kwa ajili ya madeni yaliyokwisha iva. Hatifungani hizi zitatolewa tu baada ya uhakiki kukamilika.

**Rufaa za Kodi**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2015 Bodi ya Rufaa ya Kodi imesajili jumla ya rufaa 234 na kutolea maamuzi 65 sawa na asilimia 27.8 ya rufaa zilizosajiliwa. Aidha, Baraza za Rufaa za Kodi limesajili rufaa 24 na kutolea maamuzi rufaa 26 ikijumuisha rufaa mbili zilizosajiliwa kabla ya Julai, 2014. Katika mwaka 2015/16 Bodi itaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa za kodi zilizowasilishwa na zitakazowasilishwa ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati. Bodi pia itaendelea kutoa elimu kwa wadau ambapo "Tax Law Reports" zitaendelea kutolewa ili ziweze kutumika kama rejea.

**Huduma za Kibenki**

**Benki Kuu ya Tanzania**

**75. *Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, sekta ya benki iliendelea kukua na kuimarika. Idadi ya taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu iliongezeka kutoka 57 zilizokuwepo mwezi Juni, 2014 hadi 59. Aidha, matawi ya benki yaliongezeka kutoka 634 hadi 698. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ilitoa leseni kwa taasisi nne. Taasisi hizo ni *Vision Fund Tanzania Microfinance Company* inayotoa huduma ndogo ndogo za kifedha, *Alios Finance Tanzania Limited* ambayo ni Kampuni ya karadha, *Salute Finance Limited,* na *China Commercial Bank Ltd* ambayo ni benki ya biashara.

**76. *Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wasiofikiwa na huduma za kibenki umeendelea kuongezeka kutokana na ubunifu wa mipango ya utoaji wa huduma za malipo ya reja reja kupitia simu za mikononi na huduma za uwakala wa mabenki (*agent banking services*). Ubunifu huu umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la amana za watu binafsi ambazo zimefikia shilingi bilioni 17,904.71 katika kipindi kinachoishia Machi, 2015 kutoka shilingi bilioni 15,726.5 katika kipindi kama hicho mwaka, 2014. Aidha, kutokana na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea katika utoaji wa huduma za kibenki, Benki Kuu imefanya marekebisho ya kanuni za kusimamia mabenki (*Prudential Regulations for Banking Institutions*) zilizochapishwa katika gazeti la Serikali la mwezi Agosti, 2014 toleo Na. 290.

**77. *Mheshimiwa Spika,*** takwimu za tathmini ya hali ya mabenki zinaonesha kuwa sekta ya mabenki imeendelea kuwa imara na salama, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Katika kipindi

kinachoishia mwezi Machi, 2015, kiwango cha mtaji ikilinganishwa na mali iliyowekezwa (*total capital to total risk weighted assets and offbalance sheet exposures*) kilikuwa cha asilimia 19.09 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12. Vile vile, ubora wa mikopo uliendelea kuimarika. Uwiano kati ya mikopo chechefu na jumla ya mikopo yote katika benki za biashara ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 6.52 kutoka wastani wa asilimia 8.1 wa mwezi Juni, 2014. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi (*Liquid assets to demand liabilities*) kilifikia asilimia 37.52 ikilinganishwa na asilimia 35.61 mwezi Juni, 2014 na kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20 au zaidi.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Tanzania imejiunga na mfumo wa malipo wa Jumuiya ya nchi za SADC ujulikanao kama *SADC Intergrated Regional Electronic Settlement System* (SIRESS) ili kurahisisha biashara na uwekezaji katika Jumuiya hiyo na hivyo kupanua wigo wa watanzania kufanya biashara kimataifa. Aidha, maboresho katika mfumo wa malipo kwa hundi unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili,2015 mfumo mpya wa *Tanzania Automated Clearing System* umeanza kutumika badala ya mfumo uliokuwepo awali. Maboresho haya yameongeza ufanisi mkubwa na kupunguza muda wa kusubiri malipo ya hundi kutoka siku tatu mpaka saba hadi siku moja.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo**

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha taratibu za kuanzisha Benki hii na hatua zifuatazo zimeshakamilika: ofisi kwa ajili ya kuanza shughuli za Benki hiyo imeshapatikana; Bodi ya Wakurugenzi imeshaundwa na kuanza kazi rasmi tangu Februari 2014; Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali wa Benki hiyo wameshateuliwa na kuajiriwa na tayari wameshaanza kazi tangu Septemba 2014; baadhi ya Mameneja wameshaajiriwa na taratibu za kuwaajiri maafisa wengine wa ngazi mbalimbali za chini zinaendelea vizuri; leseni ya muda ya kuanzisha Benki hiyo ya maendeleo ya kilimo imeshatolewa na Benki Kuu ya Tanzania na taratibu za kukamilisha masharti ya upatikanaji wa leseni ya kudumu ya shughuli za kibenki zinaendelea na uzinduzi rasmi unatarajiwa kufanyika mwezi Julai, 2015.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2015/16, benki imepanga kufanya yafuatayo: kupata leseni ya kudumu ya huduma za kibenki toka Benki Kuu ya Tanzania; kuzindua rasmi benki na kuanza kutoa mikopo ya maendeleo ya kilimo; kukamilisha ajira za wafanyakazi 45 waliokusudiwa kuanzisha benki; na kukamilisha Mpango Kazi, miundo ya uendeshaji na mipango ya utekelezaji ya mwaka.

**Benki ya Posta Tanzania**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014 Benki ya Posta iliendelea kusambaza huduma zake za kibenki kwa wananchi wengi zaidi ambapo hadi Disemba 2014 jumla ya matawi 28 na matawi madogo 22 yalikuwa yanatoa huduma kwa wananchi. Aidha, amana za wateja ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 169.29 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 237.53 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 40. Thamani ya mikopo inayotolewa kwa wateja iliongezeka kutoka shilingi bilioni 120.42 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 215.41 mwaka 2014 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 79. Pato ghafi lililozalishwa na benki liliongezeka toka shilingi bilioni 38.36 mwaka 2013 na kufikia shilingi bilioni 52.77 mwaka 2014.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015, Benki ya Posta imejipanga kimkakati ili kuukabili ushindaji wa kibiashara katika soko la fedha na kuongeza uwezo wake wa uzalishaji na utoaji huduma kwa kufanya yafuatayo: kuongeza mtaji kwa kubadili sheria iliyoianzisha ili kufungua milango kwa kuongeza wanahisa wengine kupitia soko la mitaji; kupanua huduma kwa wateja wengi zaidi kwa kutumia teknolojia ya TPB POPOTE; kufungua akaunti za wateja wapya 200,000; kufungua matawi madogo madogo manane wilayani ili kuwafikia wateja wengi zaidi; na kuongeza bidhaa za kibenki.

**Benki ya Maendeleo TIB**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014 Benki ya Maendeleo TIB ilikamilisha mpango wake wa marekebisho na kupata leseni kwa makampuni mawili ya TIB. Katika kipindi kilichoishia Disemba, 2014 Benki ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 10.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.6 zilizopatikana mwaka 2013. Kupungua kwa faida kumetokana na tengo la mikopo chechefu kulingana na kanuni za kibiashara. Aidha, waraka mizania wa benki ulikua na kufikia shilingi bilioni 520.1 sawa na ongezeko la asilimia 24.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 417.9 mwaka 2013. Vile vile, mikopo iliyotolewa katika sekta za ujenzi, biashara, utalii, afya, elimu na SMEs ilifikia shilingi bilioni 413.0 sawa na ongezeko la asilimia 35 ikilinganishwa na shilingi bilioni 305.8 mwaka 2013.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** dirisha la kilimo liliendelea kutoa mikopo kwa wakopaji mbalimbali kwa riba nafuu. Tangu kuanza kwa dirisha mwaka 2010 hadi kufikia Disemba, 2014 maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 299.1 yalipokelewa. Kati ya hayo, maombi ya shilingi bilioni 67.5 yaliidhinishwa. Waombaji waliopata mikopo wanatoka kwenye mikoa 22 ambayo ni Arusha, Pwani, Simiyu, Kagera, Mara, Dodoma, Mwanza, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Dar Es Salaam, Singida, Iringa, Morogoro, Tanga, Mbeya, Unguja, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Rukwa na Kigoma. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 28.1 (asilimia 54) zilitolewa kwa wakulima wadogo na wa kati wenye kampuni, shilingi bilioni 7.6 (asilimia 14.6) zilitolewa kwa taasisi ndogo

za fedha zinazokopesha wakulima wadogo na wa kati na shilingi bilioni 16.4 (asilimia 28.3) zilitolewa kwa vikundi vya kuweka na kukopa.

**Twiga Bancorp**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014 Twiga Bancorp imeendelea kutoa huduma mbalimbali za kibenki ambapo hadi Disemba, 2014 amana za wateja zilifikia shilingi bilioni 57 ikilinganishwa na shilingi bilioni 53 mwaka 2013. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wateja mbalimbali ilifikia shilingi bilioni 42 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 5 ikilinganishwa na mikopo iliyotolewa mwaka 2013. Kushuka kwa mikopo kunatokana na nguvu nyingi kuelekezwa kwenye ukusanyaji wa mikopo chechefu.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** benki kwa mwaka 2015 imepanga kufanya yafuatayo: kuongeza amana za wateja kutoka shilingi bilioni 57 hadi shilingi bilioni 77; kukuza mikopo ya taasisi kutoka shilingi bilioni 42 mwaka 2014 hadi shilingi bilioni 55; na kuongeza mapato ya taasisi kwa asilimia 40 kutokana na riba na mapato mengine yasiyo ya riba.

**Huduma za Bima**

**Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Bima imeanzisha Baraza la usuluhishi la Bima na linaendelea kupokea malalamiko ya wateja wa bima na kuyatolea ufumbuzi ili kukuza imani kwa Wananchi kuhusu huduma za bima. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima husussan Bima ya moto na majanga mengine. Lengo ikiwa

ifikapo mwaka 2017 asilimia 25 ya Watanzania wote wawe wamefikiwa na huduma za bima.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Mamlaka itafungua Ofisi ya Kanda ya Kati itakayohudumia mikoa ya Singida, Tabora na Dodoma. Lengo ni kupeleka huduma za Mamlaka karibu zaidi na Wananchi. Aidha, Mamlaka itaendelea kutoa elimu ya bima kwa umma kwa njia ya redio. Vile vile, Mamlaka itashirikiana na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kutoa elimu ya juu kwa lengo la kupata wataalam wengi wa fani ya bima.

**Shirika la Bima la Taifa**

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, mapato ya shirika kutokana na ada za bima yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 31.5 mwaka 2013 hadi shilingi bilioni 31.7 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.6. Aidha, mapato ya shirika kutokana na bima mtawanyiko yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.7 mwaka 2013 hadi shilingi bilioni 1.77 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 4.1. mapato yatokanayo na vitega uchumi yalipungua kutoka shilingi bilioni 7.3 mwaka 2013 hadi shilingi bilioni 6.3 mwaka 2014 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 14.7.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi kilichoishia 31 Desemba 2014, Shirika liliweza kulipa madai ya wateja ya shilingi bilioni 9.8 ikiwa ni asilimia 75 ya lengo la mwaka 2014. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 6.4 zililipwa kwa wateja wa bima za maisha na shilingi bilioni 3.4 zililipwa kwa wateja wa bima zisizo za maisha.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015, shirika limejiwekea lengo la kukusanya mapato ya shilingi bilioni 68.9. Kati ya hayo, shilingi bilioni 49.3 zitatokana na ada ya bima na shilingi bilioni 19.5 zitatokana na vitega uchumi vya shirika, ada za bima mtawanyo na uuzaji wa nyumba na viwanja. Aidha, shirika litaendelea na mkakati wa kuzishawishi Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kununua bima mbalimbali kutoka shirika la Bima la Taifa ili kuliwezesha kuongeza mapato.

**Mitaji na Dhamana**

**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imetekeleza yafuatayo: kusimamia Soko la Hisa la Dar es Salaam, kampuni za udalali wa uwekezaji, Mipango ya uwekezaji wa pamoja na kampuni zinazomilikiwa na wanahisa wengi; kukagua madalali na washauri wa uwekezaji ili kuona kama wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa; na kuchambua taarifa mbalimbali kuhusu Mipango ya uwekezaji wa pamoja inayoendeshwa na UTT AMIS ili kuona kama wanafuata taratibu na sheria. Aidha, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za uwekezaji na faida za kuwekeza katika Masoko ya Mitaji nchini Tanzania.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Mamlaka itaandaa taratibu za kisheria na usimamizi wa bidhaa na Huduma mpya zinazotarajiwa kuingizwa sokoni. Bidhaa hizo ni Hatifungani za

Manispaa, mifuko ya uwekezaji iliyoorodheshwa sokoni (Exchange Traded Funds), na hatifungani za akiba kwa ajili wawekezaji wadogo kwa kutumia mitandao ya simu za mikononi (Makiba Bonds).

**Soko la Hisa la Dar es Salaam**

**94. Mheshimiwa Spika,** hadi Aprili, 2015 Soko la Hisa la Dar es Salaam limeorodhesha hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 862.53. Kwa upande wa hisa za kampuni, Soko liliorodhesha hisa za kampuni za Swala Oil and Gas ltd, Uchumi Super Market na Mkombozi Commercial Bank. Aidha, hisa za benki ya walimu-Mwalimu Commencial Bank zilianza kuuzwa katika soko la awali.

**95. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2015 hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 651.9 ziliuzwa na kununuliwa. Kwa upande wa hatifungani za Serikali, hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 401.78 ziliuzwa. Aidha, mauzo ya hisa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 251.20 mwaka 2013/14 hadi shilingi bilioni 651.9 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 160. Thamani ya Soko imekua kutoka shilingi trilioni 17.3 hadi shilingi trilioni 22.7. sawa na ongezeko la asilimia 31. Mafanikio haya yametokana na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa soko, elimu kwa umma, na utendaji mzuri wa kampuni zilizoorodheshwa.

**Dhamana ya Uwekezaji Tanzania**

**96. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka miwili tangu kuanzishwa kwake, Kampuni ya UTT AMIS, ikiwa kama meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja ilijikita zaidi katika kuimarisha, kuboresha na kukuza mifuko mitano iliyorithi toka UTT ili iweze kutimiza malengo yake. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu na Mfuko wa Ukwasi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2015 mifuko hii ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi bilioni 237 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 166.1 mwezi Machi 2014 na wawekezaji zaidi ya 120,000.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI) yenye makao makuu Dar es Salaam na ofisi za kanda zilizopo Dodoma, Mbeya, Arusha, Mwanza, na Zanzibar. Taasisi imejikita katika kutoa huduma za kifedha na mikopo kwa watanzania wenye kipato cha chini na cha kati. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 6.09 ilitolewa kwa wananchi 11,591 kati ya hao wanawake ni 9,263 na wanaume ni 2,328. Aidha, pamoja na mikopo inayotolewa na UTT MFI, taasisi hii pia inatoa huduma za uuzaji wa vipande vya UTT AMIS.

**98. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT-Projects and Infrastructure Development) imejikita katika upimaji wa ardhi na kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata ardhi iliyopimwa. Hadi mwezi Aprili 2015, taasisi imepima viwanja katika maeneo ya Sengerema, Mapinga, Lindi, Morogoro, na

Bukoba na kutoa ushauri wa namna bora ya kuendesha na kusimamia soko la Mwanjelwa mkoani Mbeya. Katika mwaka 2015/16, taasisi imepanga kukuza mtaji, kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa makazi yaliyopangwa, na kuboresha miundombinu ya taasisi.

**Taasisi za Mafunzo**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo zilizo chini yake, imeendelea kutoa taaluma mbalimbali nchini. Taasisi hizo ni Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA); Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA); Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM); Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP); na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC). Katika kutekeleza jukumu hili taasisi za mafunzo zimeendelea kudahili wanafunzi na kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali nchini, kuanzisha kozi mpya ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira la ndani na nje ya nchi, kupanua huduma za mafunzo ili kuhakikisha watanzania wengi zaidi wanapata fursa ya elimu pamoja na kuendelea kuwekeza katika miundo mbinu mbalimbali ya taasisi hizi ili kuendana na ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa kila mwaka.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, udahili wa wanafunzi ulikuwa kama ifuatavyo: Taasisi ya Uhasibu Arusha wanafunzi 3,675; Taasisi ya Uhasibu Tanzania wanafunzi 8,644; Chuo cha Usimamizi wa Fedha wanafunzi 9,779; Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini wanafunzi 5,030; na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika wanafunzi 400.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 kozi mpya mbili zimeanza kufundishwa katika Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini ambazo ni: *Certificate in Development Administration and Management* na *Diploma in Development Administration and Management.* Vile vile, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, kimeendesha mafunzo ya awali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa takwimu wanafunzi waliomaliza elimu ya Sekondari na hawakufanikiwa kuingia Kidato cha Tano. Aidha, Taasisi ya Uhasibu Arusha imeanzisha kozi mpya za shahada ya Uzamili katika Ugavi na shahada ya Mafunzo Mkakati na kufungua kampasi katika mji wa Babati mkoani Manyara na jijini Mwanza.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa 2015/16, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi zake katika kudahili wanafunzi, kuboresha miundombinu pamoja na kuanzisha kozi zenye kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

**Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo**

**Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutimiza majukumu yake kupitia Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi - NBAA kama ifuatavyo: kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu nchini; kuhariri mitaala pamoja na silabi ya taaluma ya uhasibu; kuendeleza taaluma ya uhasibu; kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu; kuweka

na kusimamia viwango vya uhasibu na ukaguzi; kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu (audit quality review) ambapo hadi Aprili, 2015 *NBAA* imefanya ukaguzi katika kampuni 34 kati ya kampuni 39 uliopangwa kufanyika kwa kipindi hicho.

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutimiza majukumu yake kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu - NBS ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama ifuatavyo: kuhakiki Mipaka ya Kiutawala kwa wilaya za Gairo, Chemba, Wete na Kiteto kwa lengo la kuboresha kanza ya kijiografia inayotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kwa ajili ya maandalizi ya Sensa ya Mwaka 2022; kuhakiki mipaka ya utawala katika ngazi ya vijiji/mitaa katika wilaya za Bagamoyo na Kiteto; na kutoa Takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka na nusu mwaka, takwimu hizo zimetolewa hadi kufikia Desemba, 2014.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2007 kama mwaka wa kizio kutoka mwaka wa kizio wa 2001. Mwaka 2007 umetumika kwa vile ulikuwa na taarifa nyingi kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na tafiti za kiuchumi, kijamii na taarifa za kiutawala. Umuhimu wa marekebisho hayo unatokana na maendeleo ya kiuchumi na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mabadiliko hayo yamesababisha kuwepo kwa haja ya kufanya marekebisho na kujumuisha thamani ya bidhaa na huduma

mpya katika Pato la Taifa ambazo hapo awali hazikuwepo - mfano gesi asilia, sanaa na burudani na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa vya elekroniki zikiwemo simu za kiganjani.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na marekebisho hayo, ukuaji halisi wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 ulikuwa asilimia 7.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2012. Aidha, Pato la Taifa kwa mwaka 2013 kabla ya marekebisho hayo lilikuwa shilingi trilioni 53.2. Baada ya marekebisho hayo, ilionekana kuwa Pato la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 70 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 31.6. Vivyo hivyo, wastani wa Pato la kila Mtanzania kwa mwaka 2013 lilikuwa shilingi 1,582,797 badala ya shilingi 1,186,200 kama ilivyokisiwa awali. Kufikia mwaka 2014, Pato la Taifa lilikua na kufikia shilingi trilioni 79.4 na wastani wa pato la kila mtu lilikuwa shilingi 1,724,416 (wastani wa Dola za Marekani 1,066).

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa takwimu hizo mpya, kiwango halisi cha ukuaji wa uchumi kilikuwa asilimia 7.0 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2013. Katika kipindi hicho, shughuli za uchumi zilizokua kwa viwango vikubwa zilikuwa ni pamoja na: ujenzi (asilimia 14.1); usafirishaji na uhifadhi (asilimia 12.5); fedha na bima (asilimia 10.8); biashara (asilimia 10.0); na viwanda (asilimia 9.4). Aidha, kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo mwaka 2014 kilikuwa kidogo (asilimia 3.4) pamoja na kwamba sekta hii inaongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa asilimia 28.9. Sekta zinazofuata kwa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ni ujenzi (asilimia 12.5); biashara (10.5); na viwanda (asilimia 5.6).

**108.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2014/15 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iliendelea kusimamia michezo ya kubahatisha nchini ikiwa ni pamoja na kukusanya kodi (gaming tax) itokanayo na michezo ya kubahatisha. Hadi Aprili, 2015 jumla ya shilingi bilioni 12.63 zilikusanywa sawa na asilimia 99.63 ya lengo. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 14.62 ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 10.78 katika kipindi cha mwaka 2013/14. Aidha, Bodi ilichangia shilingi milioni 623.67 katika Mfuko Mkuu wa Serikali; sawa na ongezeko la asilimia 17.13 ikilinganishwa na shilingi milioni 532.48 ya mwaka 2013/14.

**109.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2014/15, Bodi imefanya utafiti kubaini athari ya kiuchumi na kijamii kutokana na uwepo wa michezo ya kubahatisha na hasa katika jiji la Dar es Salaam. Mapendekezo yaliyotokana na utafiti huo yamesaidia Bodi katika kuboresha utaratibu wa utoaji wa leseni mbalimbali ili kuhakikisha kwamba sekta inachangia zaidi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, katika mwaka 2015/16 Bodi inatarajia kukusanya mapato ya kiasi cha Shilingi bilioni 13.50 na hivyo kuchangia kiasi cha Shilingi bilioni 1.35 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

## Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu ya Wizara kwa Mwaka 2014/15

### FUNGU 50 - Wizara ya Fedha

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 2.53 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kodi. Vyanzo hivyo ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, leseni za minada na pango kutoka kwenye mashirika ya umma na taasisi za Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015 mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi milioni 680.36 sawa na asilimia 27 ya makadirio.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Fungu 50 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 66.67 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5.62 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 61.05 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2015, Matumizi ya Kawaida yalifikia shilingi bilioni 39.43. sawa na asilimia 59 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi bilioni 3.52 ni malipo ya mishahara kwa watumishi wa fungu hili na shilingi bilioni 35.90 ni matumizi mengineyo.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 29.80. Hadi kufikia Aprili, 2015 matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 9.26 ikiwa ni sawa na asilimia 31 ya makadirio ya matumizi ya maendeleo.

**Fungu 21- HAZINA**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Fungu 21 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 897.05. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4.04 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 662.43 ni matumizi maalum, shilingi bilioni 201.64 ni kwa ajili ya

ruzuku ya vyuo na taasisi zilizo chini ya Hazina na shilingi bilioni 28.94 ni matumizi mengineyo ya idara zilizo chini ya Fungu hili.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2015 matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 588.42. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.63 zilitumika kulipia mishahara ya watumishi waliopo chini ya Fungu 21, shilingi bilioni 13.44 zimetumika katika matumizi mengineyo ya idara, shilingi bilioni 150.49 zilitumika kulipia ruzuku ya vyuo na taasisi na shilingi bilioni 421.86 ni matumizi maalum.

**115.** ***Mheshimiwa Spika****,* bajeti ya fungu 21 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 57.37. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 40.37 ni fedha za nje, na shilingi bilioni 17.00 ni fedha za ndani. Hadi Aprili, 2015 matumizi ya fedha za maendeleo yalifikia shilingi bilioni 28.29 sawa na asilimia 49 ya makadirio.

**Fungu 22 - Deni la Taifa**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 22 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 4,354.86. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 6.58 ni kwa ajili ya mishahara na stahili za maafisa wa Serikali wa kada maalum, shilingi bilioni 4,348.28 ni kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa, pensheni, michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na matumizi mengineyo. Hadi Aprili, 2015 matumizi ya fungu hili yalifikia shilingi bilioni 3,595.75. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3.85 ni mishahara na shilingi bilioni 3,591 ni

kwa ajili ya malipo ya Deni la Taifa, pensheni na michango ya mwajiri katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 23 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 80.11. Kati ya kiasi hicho, mishahara ni shilingi bilioni 5.01 na shilingi bilioni 75.1 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Aprili, 2015 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 47.93 sawa na asilimia 59 ya bajeti ya matumizi ya kawaida.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya fungu 23 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 7.95. Hadi Aprili, 2015 matumizi yalifikia shilingi bilioni 1.98 sawa na asilimia 24 ya bajeti.

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha:**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 10 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 2.32. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 0.42 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 1.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Aprili, 2015, matumizi yalifikia shilingi bilioni 1.14.

**Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 13 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 0.19 kwa ajili ya miradi ya

maendeleo. Hadi Aprili, 2015, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 1.1 sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 144.22 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kodi ambayo yanajumuisha gawio, michango ya asilimia 10 na marejesho ya mikopo na riba kutoka kwenye taasisi na mashirika ya umma. Hadi kufikia Aprili, 2015, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 128.6, sawa na asilimia 89.2 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo makusanyo yatokanayo na gawio yalikuwa shilingi bilioni 24.5 na michango ya taasisi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ilifikia shilingi bilioni 41.7. Aidha, mapato yatokanayo na marejesho ya mikopo yalikuwa shilingi milioni 805.3.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Fungu 7 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 142.43. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 0.67 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 3.76 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 137.99 ni kwa ajili ya matumizi maalum. Hadi Aprili, 2015 matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 139.12 sawa na asilimia 97 ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya matumizi hayo mishahara ni shilingi bilioni 0.65 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 2.12 na shilingi bilioni 136.36 ni kwa ajili ya ulipaji madeni ya kimkataba na urekebishaji wa mashirika na taasisi.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Fungu 7 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 1.94. Hadi Machi, 2015 matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 0.68 sawa na asilimia 34 ya makadirio.

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Fungu 45 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 65.97 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 10.41 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 55.56 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2015, Matumizi ya Kawaida yalifikia shilingi bilioni 31.86 sawa na asilimia 48 ya makadirio.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 7.08. Hadi kufikia Aprili, 2015 matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 7.08 ikiwa ni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya matumizi ya maendeleo.

**CHANGAMOTO**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kutekeleza majukumu yake ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato;
ii. Kuchelewa kupatikana kwa fedha zilizoahidiwa na wafadhili;
iii. Wafanyabiashara kugomea matumizi ya mashine za kielekroniki za kutolea risiti (EFDs);
iv. Mchakato mrefu wa kupata mikopo ya kibiashara; na

v. Uelewa wa jamii, sekta binafsi na sekta ya umma kuhusu uendelezaji wa miradi iliyo katika Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

i. Kuendelea kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kupunguza utegemezi;
ii. Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu matumizi na faida za mashine za kielekroniki za kutolea risiti (EFDs); na
iii. Kutoa elimu kwa umma na wawekezaji kuhusu dhana ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/16**

**MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2015/16**

**Mapato**

**Fungu 50: Wizara ya Fedha**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara ya Fedha Fungu 50 inakadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi yapatayo **shilingi 2,528,002,000 (bilioni 2.53)**

**Maombi ya Fedha**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha.**

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, katika fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 71,036,206,000 (bilioni 71.03).** Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 7,624,532,000 (bilioni 7.6)**

(ii) Matumizi mengineyo – **Shilingi 63,411,674,000 (bilioni 63.41)**

**(b)** Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 370,544,428,000 (bilioni 370.54).** Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 12,000,000,000** (**bilioni 12).**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 358,544,428,000 (bilioni 358.54).**

**Fungu 21 - HAZINA:**

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 551,448,351,000 (bilioni 551.45)**. Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 62,404,177,000 (bilioni 62.4)** kwa ajili ya kulipa Mishahara ya watumishi wa Idara/ Vitengo vilivyo chini ya Fungu hili pamoja na nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Serikali.

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 489,044,174,000 (bilioni 489.04)** kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, na matumizi maalum.

**(b)** Miradi ya maendeleo - **Shilingi 680,960,366,000 (bilioni 680.96).** Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 671,926,000,000 (bilioni 671.93)**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 9,034,366,000 (bilioni 9.03)**

**Fungu 22- Deni la Taifa**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 6,254,871,977,000 (bilioni 6,254.87)**. Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 9,031,287,000 (bilioni 9.03)**

(ii) Matumizi mengineyo - **Shilingi 6,245,840,690,000 (bilioni 6,245.84)**

**Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali:**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 85,438,477,000 (bilioni 85.44).** Kati ya hizo

(i) Mishahara - **Shilingi 7,932,329,000 (bilioni 7.93)**

(ii) Matumizi mengineyo - **Shilingi 77,506,148,000 (bilioni 77.51).**

**(b)** Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 4,673,845,000 (bilioni 4.67)** Kati ya hizo:

(i) Fedha za ndani - **Shilingi 3,000,000,000 (bilioni 3).**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,673,845,000 (bilioni 1.67).**

**Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina:**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 27,257,676,000 (bilioni 27.26).** Kati ya hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 2,649,137,000 (bilioni 2.65)**

(ii) Matumizi mengineyo- **Shilingi 24,608,539,000 (bilioni 24.61).**

**(b)** Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 999,885,000 (bilioni 0.99)** Kati ya hizo:

(i) Fedha za ndani -**Shilingi 650,000,000 (bilioni 0.65).**

(ii) Fedha za Nje -**Shilingi 349,885,000 (bilioni 0.34).**

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha:**

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

**(a)** Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 2,439,537,000 (bilioni 2.43)** Kati ya hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 904,792,000 (bilioni 0.90)**

(ii) Matumizi mengineyo - **Shilingi 1,534,745,000 (bilioni 1.53).**

**Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu:**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 1,534,745,000 (bilioni 1.53).**

**(b)** Miradi ya Maendeleo, fedha za nje - **shilingi 35,768,000 (milioni 35.77).**

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fungu hili kwa mwaka 2015/16, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida **shilingi 72,152,770,000** (**bilioni 72.15**). Kati ya hizo mishahara ni **shilingi 14,209,821,000** (**bilioni 14.21**) na matumizi mengineyo ni **shilingi 57,942,949,000** (**bilioni 57.94**)

(b) Miradi ya Maendeleo **shilingi 10,667,116,000**. Kati ya hizo:

- (i) Fedha za Ndani **shilingi 8,000,000,000** (**bilioni 8**)
- (ii) Fedha za Nje **shilingi 2,667,116,000** (**bilioni 2.66**)

**HITIMISHO**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), na Mhe. Adam Kighoma Ali Malima (Mb). Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Dkt. Servacius B. Likwelile na Manaibu wake Profesa Adolf F. Mkenda, Bibi Dorothy S. Mwanyika na Dkt. Hamisi H. Mwinyimvua kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vile vile, napenda kuwashukuru Bw. Richard L. Mkumbo, Mkurugenzi wa Mipango kwa kuratibu vema maandalizi ya bajeti ya wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo,

Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha pamoja na Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa michango yao mikubwa katika kuandaa hotuba hii.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz)

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.